# SOMO MAALUM:<u>KWA NINI YESU KRISTO ALIKAA SIKU 40 TENA HAPA DUNIANI BAADA YA KUFUFUKA KATIKA WAFU NDIPO AKAPAA MBINGUNI KWA BABA YAKE!!</u>

## MAANDIKO: MDO. 1: 1 – 3.

1. **UTANGULIZI:**

Daktari Luka ambaye ndiye mwandishi wa injili ya Luka Mtakatifu na kisha akaandika kitabu chote cha Matendo ya Mitume; anatueleza kwa kina sana kwa nini Yesu alifanya ishara nyingine nyingi sana kwa **Wanafunzi** wake baada ya kufufuka na kukaa nao muda wa **siku 40** ndipo akapaa juu Mbinguni. **NENO MUHIMU NI AKIWATOKEA MUDA WA SIKU 40. MST. 3**

- Dr. Luka anafafanua zaidi kwamba Yesu alikuwa na lengo maalum la **kuwathibitishia** wanafunzi wake kwanza kwamba amefufuka kweli kweli, maana hawa wanafunzi wake walikuwa wengi wao wameshuhudia jinsi Yesu alivyoteswa na kupigwa na kisha kufa pale msalabani na baadae akazikwa; **wao kama wanadamu walio katika mwili huu, lazima tu Yesu alijua kwamba wamekata tamaa, wamechanganyikiwa na wakati mwingine alijua dhahiri kwamba wameona wamepoteza muda wao wa miaka $3^1/_2$ kutembea naye na akaishia kufa na kuzikwa kaburini**. ***Luk. 18: 31 - 34.***

- Kwa maana nzuri zaidi, wanafunzi wake (Mitume) na Wanafunzi wake wengine walihitaji uthibitisho halisi kutoka kwa Yesu mwenyewe kwamba amefufuka kweli ili kujenga imani yao upya kabla ya kuwatuma kwenda ulimwenguni mwote ili kuhubiri injili yake. ***The Apostles had to be absolutely convinced that Jesus Christ was alive in order for them to be witnesses to the rest of the world***.

- Mtume Paulo naye alilazimika kuwathibitishia Wakorintho kwamba Yesu Kristo alikufa na kisha akafufuka na alimtokea na yeye mwenyewe akiwa njiani ili kulitesa Kanisa na akabadilika; akawahakikishia wote waliomwamini Yesu Kristo kwamba kuna kuishi tena baada ya kufa katika mwili huu. ***1Kor. 15: 1 – 14; Mdo 9: 1 - 7*** Na kwamba uwezekano wa kufa katika mwili usitende dhambi tena baada ya kuokoka na kuenenda katika upya wa uzima katika mwili huu inawezekana. Ndiyo sababu nasi tunapowaambia watu wengine leo kwamba Yesu Kristo amefufuka kweli; lazima tuwe na ushuhuda katika maisha yetu kwamba Yesu Kristo yu hai ndani yetu maana ameyabadilisha kabisa maisha yetu ya kale na sasa tunaishi na kutembea katika maisha mapya na ya Utakatifu kabisa jambo ambalo hatukuliweza huko nyuma kabla ya kumwamini (kuokoka).

2. **<u>Sababu 10 zilizomfanya Yesu Kristo akae siku 40 na Wanafunzi wake baada ya kufufuka ni:-</u>**

a. **<u>Sababu ya kwanza kabisa</u>** ni ili **afute** kabisa uongo uliokuwa unaenezwa na wale askari waliopokea **rushwa** kutoka kwa makuhani ili wasambaze taarifa kwamba Yesu hajafufuka bali wanafunzi wake wamemwiba na kwenda kumzika sehemu nyingine. ***Math. 28: 11 – 15, (Math. 27: 62 – 66)***

- Kama Yesu Kristo asingeonekana **mubashara** kwa wanafunzi wake, isingekuwa rahisi kufuta uongo huu uliotungwa na kusambazwa kwa nguvu ya pesa; ndiyo sababu Yesu alilazimika kuwaambia kwamba ni mimi, nishikenishikeni!! **Luk. 24: 36 - 43**

b. **<u>Sababu ya pili</u>** kubwa ilikuwa ni **kuimarisha imani** za wanafunzi wake upya ambao walikuwa wamekata sana tamaa baada ya kushuhudia mateso (kipigo) alichokipata hadi kufa tofauti na matarajio yao. ***Luk. 18: 31 – 34, Luk. 24: 13 - 35, Yoh. 20: 24 – 29.***

c. **<u>Sababu ya tatu,</u>** Yesu alibaki ili **ajidhihirishe kwa wadogo** zake (Yakobo) waliokuwa hawaamini kwamba Yesu amefufuka, na ambao hawakwamini kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, bali ni kaka yao tu na wakawa wanaendelea na matanga**. *Math.13: 53- 59, 1Kor. 15: 3 – 5.*** (Nasi tunatakiwa tudhihirishe kwa ndugu zetu kwamba tumeokoka kweli kweli) yaani kila, wanapolinganisha maisha yetu ya zamani kabla hatujaokoka na ya sasa baada ya kokoka; waamini kuwa Yesu anaweza; na ametutokea kwa neema ya aina yake miongoni mwa Watanzania wengi.

d. **<u>Sababu ya nne</u>** Yesu alibaki ili aweke na **kuimarisha** imani ya Kiongozi atakayemwachia/atakayemkabidhi jukumu la kuchunga na kulisha kondoo zake ***(Yoh. 21: 1 – 19)***. Walikuwa wengi ndani ya mtumbwi lakini Yesu anamyookea Petro kama Kiongozi na kumhoji maswali mara tatu na kisha kumkabidhi jukumu la kuchunga na kulisha kundi na wanafunzi wenzie wote wakisikia.

***Note:*** Hakuna Kiongozi ambaye anateuliwa kwa siri, lazima atangazwe mbele ya wote atakaowaongoza nao wasikie.

- Yesu alipomwambia Petro katika mistari hii kwamba **“Nifuate”** ***Yoh. 21: 18 – 19,*** alikuwa anamaanisha kwamba maisha yake Petro na kifo chake Petro vyote vitaendana (similar) vitafanana na Yesu Kristo alivyoishi na alivyokufa. **Yesu anapokutokea katika roho yako mengine yote ya dunia hii unayaona kama mavi**!!! ***Filip. 3: 7 -8***

- Ndiyo sababu Petro akauawa kikatili na Mfalme **Nero – 64** au **65 AD** kwa kusulubiwa kichwa chini miguu juu kwenye msalaba!!! (**martyrdom)** bila kumkana tena Bwana wake Yesu. **2Petr. 1:12 – 14.** Walikuwa na tumaini (imani) kubwa kwamba hata ukifa kwa sababu ya kumtetea Yesu Kristo, utaishi pamoja naye milele na milele. Jambo hili liliwafanya wayaone maisha ya dunia hii na mateso ya dunia hii kuwa jambo la muda kitambo tu. ***2Petr. 4: 1 – 18*** (Mitume wa Yesu hawakutishwa na kifo tena hata kama kingewapata kwa sababu ya kumtetea Yesu Kristo. ***Mdo. 5: 29, 40 - 42***

e. **<u>Sababu ya tano:</u>** Alibaki na wanafunzi wake **siku 40** baada ya kufufuka ili **awathibitishie** wanafunzi wake kwamba kumtumikia Yesu katika maisha ya hapa duniani siyo chanzo cha **kufilisika** (kupoteza mwelekeo wa maisha) bali ndiyo **chanzo cha baraka tele katika maisha yetu. Yoh. 21: 1 – 14.**

***NB:*** Katika **Yoh. 21: 1 – 14 kuna surprising tano** hivi ambazo **ziliwaduwaza mitume wake :-**

i. Wingi wa samaki waliowakamata kwa muda mfupi tu.
ii. Kumuona Yesu amesimama ufuoni.
iii. Kuona moto wa makaa na samaki ameokwa juu yake kwa ajili ya wao kupata breakfast!!
iv. Kuona samaki wakubwa wamenaswa katika nyavu zao za kawaida na zisikatike
v. Yesu aliyefufuka kuwa Mtumishi wao na kisha kuwaandalia wao kifungua kinywa.

- Kwa maana nyingine; Yesu alibaki na Mitume wake na wanafunzi wake wengine **siku 40** baada ya kufufuka kwake ili kuwathibitishia kwamba wale wote watakaojitoa kumtumikia katika maisha haya; yeye Yesu atashughulika na mahitaji yao mbeleni**. *(He would take care of all their needs in the future)*.**

f. **<u>Sababu ya sita</u>** ni ile ya **kufuta mawazo** waliyokuwa **wanatamba** nayo baadhi ya wanafunzi wake kwamba Yesu sasa amefufuka; sasa ndiye atakayekuwa Mfalme wao katika Taifa la Israel na Warumi **watakiona!!!** ***Mdo. 1: 6 (Yoh. 18: 33 - 37), Yoh. 6: 10 – 15,*** (Swala la Yesu lilitikisa hata wafalme, walishona midomo; Jeshi la askari Bahalioni nzima. ***Math. 27: 27;*** waliogopa na kutambua kuwa Yesu ni mwana wa Mungu.

**Note:** **Siku zote wana wa Ulimwengu tunataka Mfalme kama huyu aliye na uwezo wa kutatua kero zetu, hasa za chakula, magonjwa,**

**maji, vita, n.k. hivyo** walimwona Yesu Kristo kwa wakati huo kuwa ndiye aliyekuwa na sifa hiyo na wala hakuhitaji apigiwe kura tena; ni kumshika kwa nguvu na kumtawaza kuwa Mfalme wa Israel!!! **Walikuwa wanatamba na kuwaambia waliowaonea na kuwadharau, sasa watakiona.**

g. <u>Sababu ya saba</u>. Alibaki na wanafunzi wake muda wa **siku 40** ili apate kuwakumbusha kuwa mafundisho aliyokuwa anawafundisha huko nyuma kumhusu yeye lazima yatimizwe juu yake wakiona ili wawe mashahidi halisi hata kama ameondoka. ***1Petr. 5:1, 2Petr. 1: 16 - 19.*** Hapa mara nyingi ndipo panapotofautisha watu wa Mungu; wengine wanafuata tuu hadithi na historia makanisani, na wengine wamekutana na Yesu halisi katika maisha yao na akawabadilsha. ***Luk. 24: 36 – 49.***

- Ilibidi akae nao na ale nao mkate na awakumbushe yote aliyowafundisha na awaonyeshe wazi kuwa ndiye yeye sasa na wala siyo Malaika.

h. **<u>Sababu ya nane na maalumu sana</u> ni Yesu kuwabariki rasmi na kuwakabidhi sasa kazi baada ya kumwelewa na kuwaahidi kuwa atakuwa pamoja nao popote watakapokwenda kumtumikia. Yoh. 14: 12, Yoh. 21 – 23, Luk. 24: 50, Huko nyuma tangu alipowaita, alikuwa hajawawekea mikono na kuwabariki kwamwe.**

**Neno lililotumika “akawabariki ni EULOGIA” Kiyunani lilikuwa na maana ya:-**

a. Mungu atafanya kazi nao popote watakapokwenda. ***Math. 28: 20, Rum. 8: 28. Dan. 3: 24 -26, Mwanz. 39: 1 – 4, 20 – 23, Dan. 3: 24 – 30.***

b. Hawahitaji nguvu zao za kimwili ili kutatua shida zao au kupigana vita. ***Mwanz. 32: 24- 30, 33:1 -4, 2Nyakt. 20: 14 – 18; au kuponya wagonjwa; Mdo. 3: 1-10, 5: 12 – 16.***
Mungu akamtegua Yakobo mguu wake na alipokutana na Esau hakuhitaji tena kupigana vita naye kimwil maana Bwana amemaliza. Sasa ni Israeli ***(Prince with God)*** na siyo Yakobo tena; hii inahitaji maelezo yakina baadae

**c.** Watakuwa na ufahamu wa hali ya juu wa mambo mengi pamoja na hekima na maarifa tofauti na hekima na maarifa tu yanayofundishwa na elimu za wanadamu; wao watafundishwa na Mungu mambo mengi sana na kuonyeshwa na Mungu mambo mengi sana. ***Dan. 1: 17, Mwanz. 41: 38 – 40, 2Wafal. 6: 11 – 17*12, Mdo. 5: 1 -11.***

**d.** Baraka za Mungu zitawafuata zenyewe. ***Zab. 23:5-6, Esta 6: 1-12, 8:15 - 17,*** tena Baraka zisizo na majuto wala ***MSOTO.***

- ***2Kor. 7:10 - (***Karama za Mungu maana yake **– zawadi za Mungu kwetu haziwezi kutusababishia majuto kamwe.**

i. __**Sababu ya tisa**__ ya Yesu kukaa na wanafunzi wake siku 40 baada ya kufufuka ni ili aondoe hali ya **matabaka waliyokuwa nayo**. ***Mdo. 1: 12 – 14, Yoh. 20: 15- 18,*** Mariamu Magdalena sasa anaweza akatumiwa na Yesu na Mitume wote wakamsikiliza; ndiyo sababu Yesu Kristo aliwatokea watu wengine tofauti tofauti na kujidhihirisha kwao. ***1Kor. 15: 5-9, Yoh. 21: 21 – 22***. Hili ni muhimu sana tukalijua hadi leo kwamba Yesu Kristo anaweza akamtokea mtu yeyote na akamtumia katika namna ya kipekee kama alivyomtokea Sauli (Paulo) ingawa huko nyuma hakuwemo katika orodha ya mitume wa Yesu. **Ni muhimu sana tangu sasa kila mteule kujaa hamu ya kutokewa na Yesu ili aimarike rohoni zaidi katika safari hii ya kwenda juu kwetu Mbinguni**

***Note: Yoh. 21: 21- 22:*** Kama Yesu asingetatua tatizo hili la Petro na Yohana kabla ya kuondoka unafikiri nini kingeendelea kati ya Petro mzee ambaye amekabidhiwa kulisha na kuchunga kondoo na Yohana aliyependwa sana na Yesu na muda wote alikuwa anakaa **ameegema** kifuani mwa yesu!!!

- Wanatheolojia wanasema hivi:- ***John 21: 21 – 22***
  **To be like Peter is Honourable and to be like John (beloved disciple is desirable, but to be in the Lord's will is profitable.** (yaani kuwa kama Petro ni **heshima,** kuwa kama Yohana **inapendeza,** bali kuwa katika mapenzi makamilifu ya Mungu **kunafaa** sana (kuna faida sana). Baada ya makemeo yale kwa Petro.
- Aliwaacha wote wakitamani kuyafanya mapenzi makamilifu ya Mungu na kuweka Kando mapenzi yao. **Zab. 40: 8**. Leo hii bado kuna mashindano ya nani bora kuliko mwingine; Yesu akitutokea kikamilifu katika roho zetu, kila mmoja atamwona ndugu yake kuwa bora kuliko yeye**. Filip. 2: 3- 4, na atakuwa na nia ya Kristo daima. Filip. 2: 5 – 8.**

__Sababu ya kumi__**. Alitaka wanafunzi wake wote waone akiinuliwa na wingu likampokea kutoka machoni pao. Mdo. 1:9.** Kuinuliwa kwa Yesu machoni pa wanafunzi wake kuliamsha ibada kubwa mioyoni mwa wanafunzi pamoja na furaha kuu sana. ***Luk. 24: 51 – 53.***

- Kumbuka kwamba katika eneo hili la Bethania ambako chini ya Bonde linaloitwa Getsemani na juu ni mlima mdogo unaoitwa mlima

wa Mizeituni (kama km. 2 tu hii kutoka katika Jiji la Yerusalemu) Yesu alianzia mateso yake hapa, na halafu saa ya kupaa anakuja hapa hapa na Wanafunzi wake wanashuhudia akipaa hapa Bethania!! **(Luk. 19: 229, 22: 39, 24: 50 – 53**). Kwa macho yao wakaona anapaa!!! Anachukuliwa juu!!! Alikuja kutoka juu na sasa anachukuliwa kurudi juu!!! Ni kitendo kilichoimarisha sana imani yao kwamba tunayo makao yetu mapya juu kama alivyokuwa amewafundisha. ***Yoh. 14: 1 – 3.***

- Kila mmoja alifurahi na kufahamu kwa kina kwamba ipo siku Yesu atakuja kuwachukua ili waende waone kwake maana hapa duniani **Yesu hakuwahi kukaribisha mtu yeyote kwake maana alikuwa hana makao!!! Math. 8:20 (Luk. 9:58).**
- Wote walioshuhudia tendo hili la kupaa kwa Yesu kwa macho yao, hatuna rekodi ya mtu yeyote kati yao aliyerudi nyuma, hata alipopitia mateso makali namna gani, alijua ni ya muda na baada ya hayo atakwenda kuishi milele na Yesu kwenye makao yake juu Mbinguni. Na kama kuna injili iliyohubiriwa kwa nguvu na Paulo ni hii" ***1Kor. 15: 50 – 58,, 1Thesal. 4: 13 – 18, Rumi 14: 7 – 9. Tukio hili liliwaondolea Mitume na Wanafunzi waliomwona akipaa hofu ya kufa kabisa katika mwili huu. Hata wale waliokuwa mwanzoni wakimwona Yesu kama mtu wa kawaida, tendo hili liliwabadilisha kabisa.***
- Yesu hakuhitaji gari la moto au farasi wa moto kuja kumchukua kama ilivyokuwa kwa Eliya - ***2Wafal. 2: 11***, yeye ndiye muumba wa nguvu zote za mvutano, alipoinua tu mikono yake; nguvu hizo zikatambua na badala ya kumshusha chini kwa sababu ni mzito, zikampandisha.
- Ni wakati wa kila mteule wa Mungu kuomba Bwana Yesu amtokee kibinafsi katika maisha yake ili awe shaidi asiyekatishwa tamaa tena na lolote atakalokutana nalo katika safari hii; alenge kwa asilimia 100% kwenda kukaa na Bwana milele na milele kwenye makao yake mazuri ajabu. ***Ufun. 21: 9 – 27.*** **Amina**

***Mungu awabariki.***

***Na***
***Askofu Dr. L. M. Mwizarubi***
***Pasaka 2021***